

MAMLAKA YA USIMAMIZI WA SEKTA YA HIFADHI YA JAMII



TAARIFA KWA UMMA

VITAMBULISHO VYA TAIFA KWA WANACHAMA WA MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII

Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), inawataka wanachama wote wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuhakikisha kuwa wana vitambulisho vya Taifa (National Identity Card). Kwani kupitia kitambulisho cha Taifa tu, mwanachama ataweza kupata huduma na taarifa zake zote muhimu zinazohusiana na masuala ya Hifadhi za Jamii kwenye mifuko yote ya hifadhi ya jamii.

Vitambulisho vya Taifa vinatolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwenye ofisi zake zilizopo kote nchini.

Ili kupata kitambulisho cha Taifa mwanachama anatakiwa awe na nyaraka na vielelezo vifuatavyo; Cheti cha kuzaliwa, Pasi ya kusafiria, Vyeti vya shule (Msingi na Sekondari), Leseni ya Udereva, Kadi ya Bima ya Afya, Kadi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi, Kitambulisho cha Kupigia Kura na Kitambulisho cha kazi. Pia atatakiwa kuzingatia kanuni na taratibu za Usajili kama zitakavyoelekezwa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa kupitia tovuti ya NIDA ambayo ni www.nida.go.tz.

Kwa maelezo au ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) kupitia namba 0656 631253 na 0715 446721 au barua pepe info@ssra.go.tz au fika ofisi za Mamlaka zilizopo Dodoma katika jengo la Mkaguzi Mkuu wa Serikali au Dar es salaam katika jengo la Alpha House barabara ya Bagamoyo.

Imetolewa na
Kitengo cha Mawasiliano
Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii

S.L.P 31846

Tovuti: www.ssra.go.tz

Dar es Salaam.

07/06/2018